JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

ARDHI BULLETIN

Issue no.02
JARIDA MAALUM
Dec. 2025

UTOAJI HUDUMA KUPITIA

# ARDHI CLINIC



Jarida Maalum

**"Hizi ni jitihada mahsusi zenye lengo la kumsogezea huduma mwananchi katika eneo lake na kwa haraka na gharama nafuu."**

— Anthony Sanga —
KATIBU MKUU





YALIYOMO

1. Madebe akabidhiwa Hati Miliki 16
2. Wanawake wanufaika na Hati Nzega
3. Mbarali changamkieni fursa - DC

# WIZARA YA ARDHI YAPIGA KAMBI YA KLINIKI ZA ARDHI MIKOANI



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Eng. Anthony Sanga (kushoto) akijadili jambo na Kamishna wa Ardhi Bw. Nathaniel Mathew (katikati) na Naibu Kamishna Bw. Hussein Sadiki Kivule - Dar es salaam.

Na Eleuteri Mangi - DSM

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepiga kambi kwenye Kliniki ya Ardhi katika mikoa mitano nchini ili kutoa huduma za ardhi kupitia zoezi la uwamuaji wa urasimishaji wa makazi ya wananchi.

Mikoa hiyo ni Dar es salaam, Pwani, Tabora Dodoma, Mbeya, Arusha, Njombe, na Shinyanga, ambapo timu kutoka Ofisi ya Wizara Makao Makuu kutoka Dodoma inashirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa eneo husika pamoja na watumishi wa Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa mkoa husika wanaendelea kutoa hatimilki za ardhi katika maeneo husika.



Katika mkoa wa Dar es salaam, timu hiyo inashirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Ilala jijini Dar es salaam ambayo imepiga kambi katika Kata ya Kivule kuendesha zoezi la Kliniki ya Ardhi na kutoa Hatimiliki za Ardhi kwa wananchi baada ya kukamilisha zoezi la ukwamuaji wa urasilishaji wa makazi ya wananchi hao.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga akaongeza mwezi mmoja kwa watumishi wanaotoa huduma za ardhi kwenye Kliniki ya Ardhi inayofanyika Kata ya Kivule Ilala Dar e salaam kuanzia Agosti 18, 2025 ili kupunguza mzingo mkubwa kwa wananchi ambao hawana hati.



Mratibu wa Urasimishaji Mkoa wa Dar es Salaam Laurent Mswani akitoa elimu ya jinsi ya kuhifadhi hati kwa mwananchi aliyefika kupata huduma katika Kliniki ya Ardhi iliyofanyika Kivule - Dar es salaam

## MBEYA

# "Tunawafuata wananchi"

## NAIBU KATIBU MKUU ARDHI



Na Eleuteri Mangi

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaendesha zoezi la Kliniki za Ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi katika maeneo yao.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Igurusi wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Bi. Lucy Kabyemera amesema katika mwezi Oktoba 2025 timu ya wataalamu kutoka wizara hiyo inaendelea kutoa huduma za Kliniki za Ardhi katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Mtwara, Njombe, Pwani na Tabora.

"Zoezi hili ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa kwa Wizara kusogeza karibu huduma za ardhi kwa wananchi, tuna ofisi Ardhi zakatika mikoa yote 26. Tumeenda mbele zaidi kwa kutoka kwenye ofisi zetu na kuwafuata wananchi na kutoa huduma za sekta ya Ardhi" amesema Naibu Katibu Mkuu Bi. Lucy.

Aidha, Wizara hiyo inatekeleza falsafa ya 4R za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo uboreshaji wa mifumo ya utendaji kazi wa utoaji huduma ambapo sasa hivi wizara inatumia mfumo wa e-Ardhi ambao unatumika kutoa huduma za masuala ya ardhi.

Mwitikio wa wananchi wa Halmashauri ya Mbarali KATIKA kata za Igurusi. Ubaruku na Rujewa ni takriban 557 wamefika na wamepata huduma katika zoezi la Kliniki za Ardhi linaloendelea wilayani humo.



ARUSHA

# SERIKALI YAENDELEA KUWEZESHA WANANCHI KUPATA HATI MILKI ZA ARDHI

Na Munir Shemweta



Serikali kupitia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kuwawezesha wananchi kupata hati milki za ardhi ili kuongeza kasi ya umilikishaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Uwezeshaji huo unafanyika kupitia mazoezi ya urasimishaji makazi holela pamoja na Kliniki Maalum za Ardhi zinazofanyika maeneo mbalimbali nchini zikiwa na lengo la kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Kwa upande wa mkoa wa Arusha inapofanyika Kliniki ya Ardhi katika kata ya Muriet, jumla ya viwanja 18,886 vimetambuliwa na viwanja 14,562 vimeidhinishwa.

Akizungumza wakati wa kliniki hiyo tarehe 16 Oktoba 2025 jijini Arusha, Mratibu wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) Bw. Elia Kamihanda amesema, kliniki hiyo ya ardhi mbali na kutoa huduma mbalimbali za sekta ya ardhi inatilia mkazo kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi hususan kwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao katika kata ya Muriet.

"Huduma hii ya kliniki ya ardhi ina manufaa makubwa hususan kwa wananchi wa Muriet waliorasimishiwa maeneo yao kwa kuwa watapata usalama wa milki yao na kuweza kusimamia haki zao kupitia nyaraka za milki" amesema Kamihanda

Amewataka wananchi wa Muriet kujitokeza kwa wingi katika kliniki hiyo ya Ardhi ili waweze kupata huduma za sekta ya ardhi sambamba na kumilikishwa maeneo yao kwa kupatiwa hati alizozieleza kuwa, zitawasaidia katika shughuli zao za kimaendeleo pamoja na kuepuka migogoro ya ardhi.

Maeneo ambayo kliniki hizo maalum za ardhi zinafanyika nchini ni Chalinze mkoa wa Pwani, Nzega Tabora, Mbarali Mbeya pamoja na wilaya ya Njombe mkoa wa Njombe. Huduma hizo zinatarajia pia kuendelea katika halmashauri ya manispaa ya Mtwara Mikindani na Peramiho, Ruvuma.

Huduma zinazotolewa kupitia Kliniki hizo Maalum za Ardhi ni utoaji hati milki za ardhi papo kwa hapo kwa waliokamilisha taratibu za umiliki, utoaji elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya mfumo wa utoaji huduma za ardhi kidigiti (e-ardhi) na usaidizi wa ufunguaji akaunti ya mwananchi katika mfumo wa e-ardhi.


# SERA YA ARDHI YATEKELEZWA KWA VITENDO: WANAWAKE NZEGA WANUFAIKA NA HATI MILIKI ZA ARDHI

Na Magreth Lyimo & Joel Magessa

Wanawake katika Halmashauri ya Mji Nzega mkoani Tabora wameanza kunufaika na azma ya serikali kuhakikisha wanamiliki ardhi kama ilivyoainishwa katika sera ya ardhi ya mwaka 1995 toleo la mwaka 2023.

Katika siku ya pili ya Kliniki ya Ardhi inayoendela katika viwanja vya Community Centre, wanawake waliokuwa wakifuatilia hati miliki za ardhi katika kliniki hiyo wamepatiwa hati zao na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi Bw. Deogratius Kalimenze.

"Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 toleo la mwaka 2023 limeweka msukumo mkubwa katika kuhakikisha usawa wa kijinsia, kwa kutambua haki za wanawake kumiliki na kurithi ardhi, pamoja na kushirikishwa kikamilifu katika maamuzi ya matumizi ya ardhi katika familia na jamii" amesema Kalimenze




Miongoni mwa wanawake waliopata hati miliki Bi. Constansia Kapama alieleza furaha yake baada ya kupokea hati miliki ya kiwanja chake, akisema hatua hiyo imempa uhakika wa umiliki na uwezo wa kutumia ardhi yake kama rasilimali ya maendeleo.

"Tunaishukuru sana Serikali kwa kutuletea huduma hii ya ardhi karibu nyumbani imeturahisishia sana, naomba niwahamasishe na wanawake wenzangu wafike kwa wingi kufuatilia hati zao" amesema Bi. Constansia.Nae Bi. Odilia Golagoza ambaye amepokea hati miliki mbili za maeneo yake aliishukuru Serikali kwa kuwawezesha wanawake kumiliki ardhi na kusema kuwa yuko tayari kuhamasisha wanawake wa Sagara wafuatilie hati zao ili waweze kuwa na umiliki wa maeneo yao.

Kwa upande wake, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora Bw. Tumaini Gwakisa amesema kuwa, Kliniki ya Ardhi ni sehemu ya jitihada za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi za kusogeza huduma karibu na wananchi, huku ikizingatia usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi kwa njia ya utoaji elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa wanawake kumiliki ardhi na umiliki wa ardhi wa pamoja kati ya mume na mke.

Kliniki ya Ardhi katika Halmashauri ya Mji Nzega imeanza tarehe 15 Oktoba 2025 na itahitimishwa tarehe 24 Oktoba 2025 ikiwa na lengo la kutoa huduma za ardhi kama Utoaji wa hati miliki za ardhi papo kwa papo, Utatuzi wa migogoro ya ardhi, Makadirio ya kodi ya pango la ardhi, Uhuishaji milki zilizoisha muda wake pamoja na kutoa Elimu na ushauri kuhusu masuala ya ardhi.

**HUDUMA ZIMERAHISISHWA!**

Tumia mfumo wa **e-Ardhi** kupata huduma **Kidijiti** https://eardhi.lands.go.tz



# DC NZEGA AHIMIZA MATUMIZI YA MFUMO WA e-ARDHI



Na Magreth Lyimo & Joel Magessa

Mkuu wa Wilaya ya Nzega mkoani Tabora Mhe. Naitapwaki Tukai amehimiza matumizi ya teknolojia kupitia mfumo wa kidigiti wa e-ardhi katika kupata huduma mbalimbali za sekta ya ardhi nchini.

Amesema, matumizi ya teknolojia kupitia mfumo wa e-Ardhi si hiari bali ni hitaji muhimu katika karne ya sasa ambapo ameongeza kuwa, mfumo huo unarahisisha utoaji wa huduma, unaimarisha uwazi na uaminifu pamoja na kupunguza gharama na muda wa upatikanaji wa huduma.

Akizindua rasmi Kliniki ya Ardhi tarehe 18 Oktoba 2025, katika Viwanja vya Community Centre Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Mhe. Tukai, aliipongeza Wizara ya Ardhi kwa ubunifu wa kusogeza huduma karibu na wananchi na kueleza kuwa, hatua hiyo inasaidia kuongeza uelewa, uwazi, na usalama wa milki za ardhi.



Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Mkoani Tabora, Mhe. Naitapwaki Tukai, akimkabidhi hati miliki mmoja wa wananchi wakati wa uzinduzi wa Programu ya Kliniki ya Ardhi uliofanyika katika Halmashauri ya Mji Nzega tarehe 18 Oktoba 2025.


"Napenda kutoa rai kwa wananchi wa Nzega kuendelea kujitokeza kwa wingi ili kunufaika na huduma hizi muhimu za umilikishaji kupitia Kliniki ya Ardhi, elimu ya mfumo wa e-Ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi," alisema Mhe. Tukai.

Akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa Kliniki hiyo Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi Bw. Deogratius Kalimenze amesema, Wizara inalenga kurasimisha vipande vya ardhi 20,000 katika kata tano za Nzega Mashariki, Nzega Magharibi, Nzega Ndogo, Kitangiri na Uchama ambapo tangu kuanza kwa Kliniki ya Ardhi tarehe 15 Oktoba 2025, jumla ya wananchi 458 wamepata huduma za elimu ya matumizi ya mfumo wa e-Ardhi, na zaidi ya wananchi 109 wamefunguliwa akaunti kupitia mfumo huo.

Aidha, viwanja 85 vimehakikiwa na kutambuliwa, hati miliki 173 zikisajiliwa ambapo 103 kati yake zimekabaidhiwa kwa wananchi, migogoro 17 imesikilizwa na 8 kati ya hiyo imetatuliwa. Pia mapato ya zaidi ya shilingi milioni 23.3 yamekusanywa kupitia makusanyo ya kodi ya pango la ardhi na ada za umilikishaji ardhi.

Kliniki ya Ardhi katika Halmashauri ya Mji Nzega itahitimishwa tarehe 26 Oktoba 2025, huku wananchi wa Nzega wakiendelea kupata huduma za umilikishaji, elimu ya e-Ardhi, ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya ardhi pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi.


# JINSI YA KUJISAJILI KWENYE MFUMO





## 1. NAMNA YA KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA eARDHI

**Fuata hatua hizi muhimu:**

1. Fungua tovuti: https://eardhi.lands.go.tz
2. Bonyeza "Jisajili" (Create Account)





3. Jaza taarifa binafsi:
   - Namba ya NIDA
   - Namba ya simu



4. **Pokea OTP** (One Time Password) kwenye namba ya simu uliyoingiza.
5. Ingiza namba hizo (OTP) ili kuendelea.
6. Weka taarifa zako zaidi (mfano, barua pepe na nywila mpya).
   - **Mfano wa nywila salama:** *Mkombozi@2025* (mchanganyiko wa herufi na alama).
7. Bonyeza "**Jisajili**" ili kukamilisha usajili.

## 2. NAMNA YA KUINGIA KWENYE MFUMO (LOGIN)

1. Tembelea https://eardhi.lands.go.tz




2. Bonyeza "**Ingia**".
3. Chagua njia ya kuingia (Namba ya simu, NIN, NIDA au barua pepe).
4. Weka:
   - Jina la mtumiaji (barua pepe au namba ya simu au NIDA).
   - Nywila (Password).
5. Bonyeza "**Ingia**" ili kufungua akaunti yako.

## JINSI YA KUOMBA HUDUMA NDANI YA MFUMO


1. Ingia kwenye akaunti yako.
2. Chagua "Maombi"
3. Chagua huduma unayotaka (mfano: "OmbaHatimiliki").
4. Bonyeza alama ya + (jumlisha) kisha jaza fomu ya maombi.
5. Ambatanisha nyaraka.
6. Thibitisha taarifa na bonyeza "Tuma".
7. Subiri ujumbe wa uthibitisho au maelekezo zaidi.

## 3. JINSI YA KUBADILI NYWILA (PASSWORD RESET)

1. Tembelea https://eardhi.lands.go.tz.
2. Bonyeza "**Ingia**".
3. Chagua "**Badili Nywila**".



4. Ingiza taarifa (NIN, barua pepe au namba ya simu) kulingana na chaguo lako.



5. Bonyeza "**Badili Nywila**".
6. Fungua simu/barua pepe yako upate ujumbe wenye link ya kuweka nywila mpya.
7. Tumia nywila mpya kuingia tena kwenye mfumo wa e-Ardhi.

**Unaweza pia kufuatilia hali ya ombi lako kwa kubonyeza vidoti vitatu vilivyo upande wa kulia wa muamala husika.**

## JINSI YA KUFUATILIA MAOMBI YAKO

1. Ingia kwenye akaunti yako. Bonyeza "Maombi".
3. Utaona taarifa za:
   - Hali ya maombi
   - Hatua inayofuata.
   - Malipo au nyaraka zinazokosekana.

Taarifa pia zinaweza kukufikia kupitia SMS au barua pepe.

## WASILIANA NASI:

**Simu: 0717722449 /071468162/ 0625652084/0755762375/0713986261**
**Email: support@lands.go.tz**
**Tovuti: https:/eardhi. lands.go.tz**
**Au tembelea ofisi ya ardhi ya wilaya au mkoa wako kwa msaada zaidi.**

## ELIMU KWA UMMA

Elimu kwa umma kuhusu masuala ya ardhi inaendelea kutolewa kupitia vipindi maalum vya redio mkoani Njombe, sambamba na Kliniki ya Ardhi inayoendelea kufanyika mkoani humo.



## MADA ZILIZOJADILIWA

Kupitia vipindi hivyo, wananchi walielimishwa kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi kwa hati halali, taratibu za umilikishaji, pamoja na huduma mbalimbali zinazotolewa kwenye kliniki hiyo ikiwemo ushauri wa kisheria, upimaji wa ardhi na uthibitishaji wa umiliki.

## MATARAJIO

Lengo kuu la elimu hii ni kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao katika matumizi bora ya ardhi, sambamba na kuhamasisha ushiriki wao katika huduma zinazotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.



Kamishina wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Njombe Fulgence Kanuti (kulia)akimkabidhi Hati 16 Mwekezaji wa Kilimpo cha Parachichi Bw. Eligius Wella (Madebe) 11 Oktoba 2025 ofisi za Kifanya Mkoani Njombe

# MADEBE AKABIDHIWA HATI MILIKI 16.

Na Jeston Kihwelo

Katika jitihada za Serikali kuboresha usimamizi wa ardhi na kuhakikisha wananchi wanamiliki maeneo yao kisheria, Bw.Eligius Wella (Madebe), mkazi na mwekezaji katika kilimo cha parachichi kijiji cha Kifanya, ni miongoni mwa wananchi waliopatiwa hati miliki katika Kliniki ya Ardhi iliyofanyika Kijiji cha Kifanya Mkoani Njombe.

Mwekezaji huyo alikabidhiwa jumla ya hati miliki 16 na Kamishina wa Ardhi Msaidizi Bw.Flugence Kanuti kwa maeneo mbalimbali anayoyamiliki, hatua ambayo imepongezwa kama mfano wa kuigwa kwa wananchi wengine wenye maeneo zaidi ya moja.

Zoezi la utoaji wa hati hizo lilifanyika kupitia kliniki ya Ardhi iliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Kufanyika Maeneo ya Matembwe,Kifanya na Makambambo mkoani Njombeambapo wananchi wote waliokamilishiwa nyaraka za umiliki walihamasishwa kufika kuchukua hati zao.

Kliniki ya Ardhi Mkoani Njombe ilifanyika kuanzia Tarehe 8 hadi tarehe 17 Oktoba 2025, na ililenga kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia msaada wa kisheria na kitaalamu kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria kutoka Wizara ya Ardhi akizungumza na wananchi kabla ya kuanza Kliniki hiyo.



Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Njombe, Fulgence Kanuti akitoa maelezo ya awali kabla ya Kliniki ya Ardhi



Mwananchi mkazi wa Njombe aliyefika katika Kliniki akikagua nyaraka alizopewa kwa ajili ya umilikishaji ardhi.



Msajili wa Hati Msaidizi Mkoa wa Njombe Bw. Benedict Nsaji, akimkabidhi mwananchi Hati baada ya taratibu zote kukamilika tarehe 10 Oktoba 2025, Mkoani Njombe

# WANANCHI 594 WAKABIDHIWA HATI MILIKI KATIKA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA

Na Jeston Kihwelo

Wananchi 594 wamekabidhiwa hati miliki za ardhi katika mkoa wa Njombe, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja katika sekta ya ardhi.

Huduma hiyo inatolewa kupitia Kliniki za Ardhi zilizofanyika katika kata za Matembwe, Kifanya na Ilangamoto mkoani Njombe.

Akizungumza na waandishi wa habari tarehe 10 Oktoba, 2025, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Njombe, Fulgence Kanuti, alisema zoezi hilo ni sehemu ya juhudi za Serikali kuhakikisha wananchi wanamiliki ardhi kihalali na kupata nyaraka rasmi.

"Katika maeneo yote matatu, jumla ya viwanja takribani 4,800 vimepimwa kupitia mazoezi ya urasimishaji yaliyofanyika kwa ushirikiano kati ya ofisi ya ardhi mkoa wa Njombe, Halmashauri ya Mji na Wilaya ya Njombe pamoja na sekta binafsi za upangaji na upimaji," alisema Kanuti.

"Matarajio yetu ni kuwafikia wananchi wote hawa 4,800 ambao maeneo yao tayari yamepimwa, ili kuwamilikishia na kuwapatia hati miliki za ardhi zitakazowasaidia kiuchumi," aliongeza Kanuti.

Kwa mujibu wa Kanuti, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na kampuni binafsi imeendelea kurasimisha maeneo ya wananchi kwa mujibu wa sheria, huku huduma ya kutoa elimu ya ardhi ikiendelea kutolewa kwa wananchi wote waliotembelea kliniki hizo.

"Migogoro mingi ya ardhi Njombe ni midogo midogo na inasababishwa zaidi na ukosefu wa uelewa. Kupitia elimu tunayotoa katika kliniki hizi, migogoro mingi imekuwa ikitatuliwa mara moja," amesema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Lucy Saleko, amesema ameridhishwa na mwamko mkubwa wa wananchi wa Njombe kushiriki katika zoezi hilo la urasimishaji.

"Wananchi wengi wamejitokeza kufuata huduma za upimaji na usajili wa hati. Wale waliokuwa tayari wamelipia na kujaza nyaraka walipatiwa hati zao papo hapo," alisema Saleko.

Baadhi ya wananchi walionufaika na zoezi hilo waliipongeza serikali na kuonesha furaha yao kwa Serikali kuwapelekea huduma hizo karibu. Riziki Nisilu, mkazi wa Njombe, amesema huduma hiyo imekuwa na manufaa makubwa kwao.

"Tunashukuru kwa huduma hii ya urasimishaji wa ardhi. Kupata hati miliki kutatuwezesha kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha na kukuza uchumi wetu," alisema.

Huduma katika kliniki ya ardhi zilihitimishwa mkoani Njombe tarehe 17 Oktoba 2025 ambapo juhudi za Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi zifanikisha kufikiwa kwaa wananchi wengi waliojitokeza kuja kupata huduma mbalimbali za sekta ya ardhi ikiwepo upatikanaji wa Hati na kutatuliwa migogoro yako.

> "Wananchi waliokuwa tayari wamelipia na kujaza nyaraka walipatiwa hati zao papo hapo,"
> **KANUTI**

# NDEMANGA AWAASA WAZEE KUACHA KUUZA ARDHI KIHOLELA

Na Lusajo Mwakabuku

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Mheshimiwa Shaibu Issa Ndemanga, amewaasa wakazi wa Wilaya ya Bagamoyo hususan Halmashauri ya Chalinze kuacha tabia ya kuuza maeneo yao tena kwa bei isiyoendana na soko kwa ajili ya kutatua changamoto za muda mfupi bila ya kuwa na uelewa wa kutosha juu ya milki zao.



Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani Bwana Rugambwa Banyikila (Kulia) akimpa maelezo Mgeni Rasmi Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Mheshimiwa Shaibu Issa Ndemanga siku ya uzinduzi wa Kliniki ya Ardhi Halmashauri ya Chalinze tarehe

Ndemanga ameyasema hayo leo 11/10/2025 wakati akizindua rasmi Kliniki ya Ardhi inayoendeshwa katika Halmashauri ya Chalinze ikiambatana na maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja katika uwanja wa Ofisi za Halmashauri hiyo akiwataka wana Chalinze wajitokeze kwa wingi si kwa ajili ya kupata hati peke yake bali elimu pia juu ya ardhi ili watambue thamani halisi ya maeneo yao.

“Naomba kuwaambia wazee wangu mliopo hapa na wengine muwapelekee habari hii, acheni kuuza maeneo yenu kiholela. Hii Pwani yote sasa hivi soko linaendelea kukua kila siku, kumbukeni Dar es salaam imeshajaa na sasa inapumulia huku kwetu, kuna nafasi nyingi za uwekezaji na utajiri wa kutosha iwapo mtaitumia rasilimali hii ipasavyo” Alisema Mkuu wa Wilaya huyo.

Aidha Mheshimiwa Ndemanga akaongeza kuwa iwapo wapo wakazi wenye maeneo na wanadhani hawawezi kuyaendeleza basi wafike katika Ofisi za Ardhi au kupitia Kliniki inayoendelea ili waweze kupatiwa elimu ya thamani ya maeneo yao hivyo waweze kuuza kwa bei sahihi ama kuingia ubi ana wawekezaji huku wakiendelea kuyamiliki maeneo yao.

“Kuna mzee mmoja hapa Jirani nimeshuhudia Watoto wake wanakuja kulalamika kuwa kauza eneo kwa shilingi Laki Moja na Nusu! Hii ni fedha ndogo sana ambayo haiendani na thamani ya eneo hasa wakati huu ambapo nchi yetu imefungua milango kwa wawekezaji na hapa kwetu ni sehemu muhimu kwa sekta hiyo” aliongeza Ndemanga.

Akisoma taarifa ya utangulizi ya Mkurugenzi wa Wilaya hiyo, Mkuu wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri ya Chalinze Bwana Deo Msilu alisema huduma ya Ardhi Clinic katika Halmashauri ya wilaya ya Chalinze inayoendeshwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Kamishina wa Ardhi msaidizi Mkoa wa Pwani ilianza tarehe 7/10/2025 na itafanyika kwa wiki mbili.

Akiongelea zoezi la Uboreshaji wa Usalama wa Milki za Ardhi katika Halmashauri ya Chalinze lililoanza rasmi mnamo tarehe 27/06/2024, Bwana Msilu alisema Kliniki hii inaendeleza zoezi hilo ambalo hadi kufikia tarehe 30/3/2025, Kata tatu za Bwilingu, Pera na vigwaza, vipande vya ardhi 24,730 vimeshatambuliwa na kupimwa viwanja 23,936. Zoezi hili limekuwa na mwitiko mkubwa sana kwa wananchi ambao walikuwa na kiu ya muda mrefu ya kupimiwa maeneo yao ambao wengi wao hawana uwezo wa kumudu gharama za upangaji na upimaji

Bwana Msilu alisema zaidi ya wananchi 500 hadi sasa wamehudumiwa kupitia kliniki hii ambayo imerahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za kisekta kwa wananchi katika maeneo haya zikiwemo utoaji wa elimu ya ardhi, upokeaji wa kero za wananchi, utatuzi wa migogoro, umilikishaji na ugawaji wa hati miliki za ardhi zao ikitumia mfumo wa kisasa wa eArdhi ambao umerahisisha utendaji kazi za upangaji, upimaji na umilikishaji.

**“Dar es salaam imeshajaa na sasa inapumulia huku kwetu, kuna nafasi nyingi za uwekezaji na utajiri wa kutosha iwapo mtaitumia rasilimali hii ipasavyo”**



# MBARALI WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA HATI KUPITIA KLINIKI ZA ARDHI

By Eleuteri Mangi

Mkuu wa wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya Brigedia Generali Maulid Surumbu amewataka wananchi wa wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya kutumia vyema Kliniki ya Ardhi inayofanyika wilayani humo kujipatia huduma za sekta ya ardhi ikiwemo hati milki za ardhi ili ziweze kuwasiadia katika shughuli zao za kiuchumi.

"Ardhi ikipata thamani unaweza kukopea, huwezi kwenda kukopea ardhi ambayo haina hati, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani alisema kila kipande cha ardhi cha Tanzania ambacho kinamilikiwa na mtanzania, ni muhimu kitambuliwe, kipimwe na apate Hati Miliki ya Ardhi" amesema Brigedia Generali Surumbu.



Akikabidhi hati za umiliki wa ardhi za kielekroniki kwa wananchi wa Kata ya Igurusi Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya Oktoba 18, 2025, Mkuu wa Wilaya hiyo amempongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiboresha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kutekeleza maajukumu yake kwa kuwapeleka wataalam wake kufanya kazi karibu na wananchi wa Igurusi.

Brigedia Generali Surumbu amesema, zaidi ya viwanja 30,700 vimerasimishwa, hati zimeanza kuandaliwa na kutolewa ambapo kwa sasa huduma za ardhi zimesogezwa kwa wananchi na hivyo kupungunga gharama na muda kwa kuifuata huduma hiyo Wilayani na Mkoani.

Kwa mujibu wa Brigedia Generali Sarumbu, serikali inaendelea kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi hatua inayowarahisishia kupata Hati Miliki za Ardhi wakiwa katika maeneo yao badala ya kusafiri umbali mrefu kwenda kupokea hati hizo Ofisi za Ardhi za Mkoa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ramani kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Bw. Joseph Ikorongo amesema wananchi wa Mbarali wamehamasishwa na kuhamasika baada ya kufanyiwa urasimishaji kwa nyakati tofaurti tofauti na zaidi ya wananchi zaidi ya 1000 wameshasikilizwa na kupapa huduma kwenye maeneo ya Igurusi, Rujewa na Ubaruku katika halmashauri ya Mbarali.

"Huduma za Hati za umiliki wa ardhi umerahisishwa ambapo wizara imetengeneza mfumo wa e-Ardhi ambao ukiweka maombi yako ndani ya muda mfupi unapata hati yako ndani ya muda mfupi". Amesema Bw. Ikorongo.

Gabriel Kamwela na Neema Mkwama ambao ni miongoni mwa wananchi waliopata hati milki za ardhi katika Kliniki ya Ardhi Mbarali wamesema kuwa kupata hati ya ardhi kwa sasa imekuwa rahisi kwa kuwa huduma ya imesogezwa karibu na wananchi jambo walilolieleza limepunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

# Matukio katika Picha



Afisa Ardhi kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Bw. Daniel Bhoke, akitoa maelekezo kwa wananchi waliofika kupata huduma kupitia Kliniki ya Ardhi inayoendelea katika Halmashauri ya Mji Nzega tarehe 18 Oktoba 2025.



Mthamini Mkuu Msaidizi Dkt. Adam Nyaruhuma akizungumza na wananchi Mtaa wa Ilangamoto Makambako.



Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi Bw. Deogratius Kalimenze akizungumza na wananchi wakati akitoa elimu ya umilikishaji.



Wananchi wengi walijitokeza katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kumilikishiwa maeneo yao wakiwemo akina mama



Huduma mbalimbali zikiendelea kutolewa kwa wananchi walliojitokeza katika Kliniki mbalimbali zilizokuwa zikiendelea nchini.



Wataalam kutoka Ofisi ya Ardhi Chalinze wakitoa maelezo mbele ya mgeni rasmi aliyezindua kliniki hiyo mwezi Novemba 2025.



Tukio la kukabidhiwa hati likiendelea katika Kliniki iliyofanyika Nzega Mkoani Tabora